# DHAMBI SABA ZA KUFISHA
**Na Ndugu Christopher Mwakabanje**

SEHEMU II

Katika somo lililopita tumeangalia aina tatu za machukizo yanayosababishwa na ulimi. Ebu sasa na tuyachunguze yale manne mengine yaliyosalia katika Mithali 6:16-19. (1) Moyo uwazao mawazo mabaya, (2) Macho ya Kiburi, (3) Mikono imwagayo damu isiyo na hatia na (4) Miguu iliyo myepesi kukimbilia maovu.

## MOYO UWAZAO MAWAZO MABAYA

Moyo ndio chimbuko la mambo yote, ingawa viungo vingine vya mwili hushirikishwa tu katika kutekeleza azima ya moyo. Mara nyingi moyo unapotajwa katika Biblia ni akili inayolengwa. Tabia njema au mbaya ya mwanadamu ni matokeo ya akiba iliyohifadhiwa moyoni. "*Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo; maana ndiko zitokako chemichemi za uzima*." Yesu akizungumzia kuhusu mambo yamtiayo mtu unajisi alisema, "*Kwa maana ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo mabaya, uasherati, wivi, uuaji, uzinzi…*" (Mk.7:21-23). Mtu hawezi kuwaza mema ikiwa moyo wake una akiba mbaya (Math.12:34). Mungu huzingatia na kuangalia jinsi moyo wa mwanadamu ulivyo na wala si nje (1 Sam.16:7).

Kipaumbele kwa wanawake wanaomcha Mungu ni kujipamba utu wao wa ndani na wala si wa nje (1 Pet. 3:3,4). Tunapaswa kuzingatia yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo ya staha, haki, safi, yoyote yenye kupendeza, yoyote yenye sifa njema, ukiwapo wema wowote, ikiwapo sifa nzuri yoyote, hivyo basi mioyoni mwetu nafasi ya kuwaza maovu haitakuwepo kabisa (Wafilipi 4:8). Tunapotegemea wanadamu, mali, n.k., mioyoni mwetu tunaweza kudanganywa hata kujiona kuwa salama na kuacha kutenda mapenzi ya Mungu (Yer.17:9,10). Moyo unaweza kudanganywa na dhambi hata kufanywa kuwa mgumu usiweze tena kupokea maonyo ya Bwana (Ebr.3:13).

## MACHO YA KIBURI

Hakuna hata jambo moja jema lililotajwa katika Maandiko Matakatifu litokanalo na kiburi! Kuna msemo unaosema kwamba "Macho ni madirisha ya nafsi ya mtu." Hivyo basi, macho ya kiburi hudhihirisha moyo ulioathiriwa na kiburi. Mungu huwapinga wenye kiburi, bali huwapa neema wanyenyekevu wa moyo (Yakobo 4:6). Mtu anayefundisha elimu nyingine, wala hayakubali maneno yenye uzima ya Bwana, wala mafundisho yapatanayo na utauwa, amejivuna; wala hafahamu neno lolote (1 Tim.6:3,4). Hatupaswi kufikiri kwamba tunafahamu zaidi ya Mungu! Mambo anayotueleza Mungu ni bora kuyatenda pasipo tashwishi yeyote. Kiburi hutangulia maangamizi, na roho inayojiona kuwa bora kuliko wengine hutangulia maanguko (Mithali 16:18).

Wakristo wa Korintho walijivunia karama walizopewa na Roho wa Mungu kupitia mikono ya Paulo (linga. Mdo. 8:14-18; Rum.1:11; 2 Tim.1:6). Ingawa hawakupata karama hizo kwa uwezo wao, kila mmoja alijiona bora kuliko mwingine. Walisahau kusudi zima la karama hizo ambalo lilikuwa ni kuimarisha kanisa la Kristo. Walipungukiwa na karama kuu ambayo ni upendo! "*Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi*

*kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya, haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli*" (1 Kor.13:4-6). Tukimpenda Mungu tutanyenyekea na kuzishika amri zake (Yoh.14:15). Tutamtumkia Mungu pamoja na wanadamu wenzetu katika kicho cha Mungu. Yesu ni mfano mzuri sana kwetu kwani yeye alipokuwa hapa duniani daima alinyenyekea chini ya mapenzi ya Baba yake na kuwatumikia wengine (Yoh.6:38; 4:34; Filp.2:5-8; Math.11:28-30; 26:39-44; 20:28).

MIKONO IMWAGAYO DAMU ISIYO NA HATIA

Ni jambo linalofurahisha kutambua kwamba kazi ya mikono ni kutumikia viungo vingine vya mwili. Faida inayozalishwa na mikoni ni kwa ajili ya mwili mzima! Ni dhahiri kwamba mkono hauwezi kujihudumia au kujidhuru wenyewe. Kama ilivyo kwa viungo vingine vya mwili, tunaweza kuiitumia mikono yetu kwa mambo mema. Katika Sheria ya Musa mtu aliyemwaga damu isiyo na hatia adhabu yake ilikuwa ni kifo (Lawi 24:17; Kutoka 21:12). Iwapo mauti ilitokea kwa bahati mbaya, ilimlazimu mtuhumiwa kujiokoa kwa kukimbilia katika mji mmojawapo wa makimbilio (Yoshua 20:3-8; Hesabu 35:10-34). Uhai wa mwanadamu una thamani kubwa kwa kuwa roho ya mwanadamu ni mfano na sura ya Mungu (Mwanzo 9:6). Katika Agano jipya serikali zimekabidhiwa jukumu hilo la kutoa hukumu za haki juu ya watu wanaomwaga damu isiyo na hatia. "*Kila mtu na aitii mamlaka iliyo kuu; kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu; na ile iliyopo umeamriwa na Mungu. Hivyo amwasiye mwenye mamlaka hushindana na agizo la Mungu; nao washindanao watajipatia hukumu. Kwa maana watawalao hawatishi watu kwa sababu ya matendo mema, bali kwa sababu ya matendo mabaya. Basi wataka usimwogope mwenye mamlaka? Fanya mema, nawe utapata sifa kwake; kwa kuwa yeye ni mtumishi wa Mungu kwako kwa ajili ya mema. Lakini ufanyapo mabaya, ogopa; kwa maana hauchukui upanga bure; kwa kuwa ni mtumishi wa Mungu, amlipizaye kisasi mtenda mabaya kwa ajili ya ghadhabu*" (Rumi 13:1-4)

Sifa zilizo nyingi za mwanamke mwema katika Mithali 31:10-31 zinahusisha mikono: (1) Hufanya kazi yake ya mikono kwa moyo – mstari 13; (2) Huangalia shamba, akalinunua kwa mapato ya mikono yake – mstari 16; (3) Hutia mikono yake nguvu – mstari 17; (4) Hutia mikono yake katika kusokota; na mikono yake huishika pia – mstari 19; (5) Huwakunjulia maskini mikono yake …huwanyoshea wahitaji mikono yake – mstari 20; na (6) Hupata mapato ya mikono yake, na matendo yake yamsifu malangoni – mstari 31. Hata kwa kutumia sindano ya mkono Dorkasi aliweza kufanya mema mengi kwa Wakristo wanzake (Mdo. 9:36-43).

Yesu kwa mikono yake aliweza hata kuwaosha miguu wanafunzi wake (Yohana 13:5-15). Aliweza kuwagusa wakoma ambao hapo kabla hawakuguswa na mtu yeyote (Mathayo 8:3; Lawi 13:45,46). Kwa mikono ya watu wabaya wakamwua, lakini yeye hakurudisha mabaya (1 Pet.2:21-23; Lk.23:34; Mdo.2:23). Petro alimkata sikio mtumishi wa kuhani, lakini Yesu kwa mikono yake akalirejeza sikio mahali pake ((Yoh.18:10; Lk.22:51).

MIGUU ILIYO MWEPESI KUKIMBILIA MAOVU

Isaya akizungumzia uovu wa Yuda, anasema, "*Miguu yao hukimbilia mabaya, nao hufanya haraka kumwaga damu isiyo na hatia…*" (Isa. 59:7-8). Dhambi zote Bwana anazichukia, lakini inaonekana kuchukizwa zaidi na hizo zinazotendwa kwa makusudi kabisa. Wepesi wa miguu si

suala la miguu inayokimbia haraka, bali ni miguu iliyo tayari daima yenye shauku ya kutenda maovu. Hatupaswi pia kuwaunga mkono watu waovu, tusije tukashiriki dhambi zao (Mithali 1:15,16).

Ili miguu yetu isipotoke, tunapaswa kujifunza na kuongozwa na Neno la Mungu (Zaburi 119:101, 105). Tukiijua Injili itatuongoza katika nuru ya Mungu na kutuonya tujiepushe na mabaya (Mdo.26:18; 2 Pet.1:19). Ayubu akizungumzia uadilifu wake alisema, “*Nalikuwa macho kwa kipofu, nalikuwa miguu kwa aliyechechemea*” (Ayubu 29:15). Aliwafundisha wengine ukweli wa neno la Mungu na kuwaimarisha waliovunjika moyo. “*Jinsi ilivyo mizuri juu ya milima miguu yake aletaye habari njema, yeye aitangazaye amani, aletaye habari njema ya mambo mema, yeye autangazaye wokovu, auambiaye Sayuni, Mungu wako anamiliki*!” (Isaya 52:7; Lk.1:79; Rum.10:17; Dan.12:3).

**kapalapala@yahoo.com**
**www.kanisalakristo.com**